JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TAARIFA YA USHIRIKI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA MKUTANO WA KIMATAIFA WA KUMI (10) WA EITI ULIOFANYIKA *BRUSSELS,* UBELGIJI (*BELGIUM*) TAREHE 08-10 OKTOBA, 2026

(*EITI GLOBAL CONFERENCE*, 2026)

DODOMA

OKTOBA, 2026

1.0 UTANGULIZI

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tukiwa Nchi Mwanachama wa *Global Extractive Industries Transparency Initiative (EITI)*, tulishiriki katika Mkutano wa Kumi wa Kimataifa wa *EITI* (*10th EITI Global Conference, 2026*), uliofanyika **tarehe 8 na 9 Oktoba, 2026,** Jijini ***Brussels, Ubelgiji.*** Ujumbe kutoka Tanzania uliongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ya TEITAC **Mhe. Balozi Wilson Mutagaywa Kajumula Masilingi**, akimuwakilisha Waziri wa Madini, **Mhe. Anthony Peter Mavunde (Mb)**. Wajumbe katika ujumbe wa Tanzania walioshiriki katika mkutano huo ni hawa wafuatao: Mjumbe wa Kamati ya TEITAC **Bw. Adam Abraham Anthony;** Katibu Mtendaji wa TEITAC **Bi. Mariamu Salehe Mgaya**; Meneja wa Uwazi na Uwajibikaji **Bw. Erick Peter Ketagory**; Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria **Bi. Julieth Nimrodi Moshi** na Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu **Bw. Bakari Issa Birika**.

Mkutano huo, ulioandaliwa na Sekretarieti ya EITI kwa kushirikiana na Serikali ya Ubelgiji. Kauli mbiu ya Mkutano huo ilikuwa ni (*Transparency for Shared Prosperity*) inayosisitiza umuhimu wa **Uwazi katika Sekta ya Uziduaji kwa Ustawi wa Pamoja**. Mkutano huu hufanyika kila baada ya Miaka Mitatu (3) Mkutano wa tisa (9) ulifanyika Mwaka 2023 Dakar, Senegal.

Lengo la Mkutano huo ilikuwa ni kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa Sera za kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Sekta ya Uziduaji; Usimamizi wa Mapato yatokanayo na Rasilimali hususan Madini, Mafuta na Gesi Asilia na kuimarisha juhudi za kupunguza hatari za rushwa. Aidha, kuimarisha ustahimilivu katika kujenga uwezo wa Nishati inayotokana na Teknolojia rafiki kwa mazingira na bei nafuu; kuboresha ukusanyaji wa mapato ya serikali; na kuhakikisha wananchi kwa ujumla wao wananufaika na maliasilia za nchi zao.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau zaidi ya 1,000 kutoka nchi zaidi ya 50; Umoja wa Mataifa; Jumuiya ya Nchi za Ulaya; wakiwemo wawakilishi wa Serikali, Kampuni za Uziduaji, Mashirika ya Kiraia na Washirika wengine wa maendeleo.

Ushiriki wa Tanzania katika mkutano huo ulitoa fursa ya kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi nyingine, kubadilishana mbinu bora za utekelezaji wa viwango vya Kimataifa kuhusu Uwazi na Uwajibikaji katika shabaha ya kukuza uchumi; kuongeza Ajira na kupambana na Umaskini.

2.0 UFUNGUZI

Mkutano ulifunguliwa rasmi tarehe **8 Oktoba, 2026** na **Mhe. Maxime Prevot,** Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimaendeleo wa Serikali ya Ubelgiji (*Deputy Prime Minister and Minister for Foreign Affairs, European Affairs and Development Cooperation, Government of Belgium*). Mhe. Maxime Prevot aliwakaribisha Washiriki wote Ubelgiji na kuwahakikishia usalama. Aidha, katika hotuba yake alieleza umuhimu wa Uwazi na Uwajibikaji katika maendeleo ya kiuchumi Duniani, hasa wakati huu wa uhitaji mkubwa wa Madini ya Kimkakati (*Critical Energy Transition Minerals*) ambayo ni muhimu sana. Aliahidi kuwa Ubelgiji ipo tayari kushirikiana na EITI katika kuhakikisha Nchi zenye Madini hayo muhimu na Nchi zenye uhitaji wa Madini hayo zinanufaika kwa maslahi ya wananchi wa nchi husika.

Aidha, Kabla ya Mkutano wa Kimataifa wa EITI kuanza rasmi, tarehe **8** na **9 oktoba, 2026,** ilifanyika mikutano kadhaa kuanzia tarehe **5** hadi **7 Oktoba, 2026**, Ujumbe wa Tanzania tulishiriki katika mikutano kadhaa kwa lengo la kubadilishana uzoefu wa namna bora ya utekelezaji wa shughuli za Uwazi na Uwajibikaji katika usimamizi endelevu wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia, kwa shabaha ya kuongeza Ajira; Mapato ya Serikali; kudhibiti Rushwa na kupambana na Umaskini.

3.0 MAMBO MUHIMU YALIYOJADILIWA

3.1 Ushiriki wa Wazawa katika sekta ya Uziduaji (Local content) na Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (*Corporate Social Responsibility (CSR)*)

Washiriki walipeana uzoefu na kusisitiza umuhimu wa kuhakikisha kuwa Wazawa wananufaika na Maliasili za Madini, Mafuta na Gesi Asilia kupitia Ajira, kutokana na utoaji wa huduma na uuzaji wa bidhaa ambazo zinazozalishwa na Kampuni zinazojihusisha na Utafutaji au Uchimbaji wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Aidha, ilisisitizwa kuwa ushiriki wa Wazawa (*Local Indigenous Communities*) katika shughuli za kiuchumi zinazohusiana na Uziduaji ni muhimu na ifanyike kwa Uwazi na Uwajibikaji. Hii itaongeza fursa za Kiuchumi kwa Kukuza biashara za ndani, kudhibiti Rushwa na kuhakikisha kuwa manufaa yatokanayo na Rasilimali hizo yanawafikia wananchi wote

Aidha, ilisisitizwa Nchi Wanachama wa EITI kuhakikisha zinatunga Sera na kuzitekeleza ipasavyo kwa kuzingatia Sheria na mifumo ya usimamizi inayowezesha ushirikishwaji wa Wazawa katika sekta ya uziduaji. Vilevile, ilielezwa umuhimu wa Makampuni kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji kwa jamii zinazozunguka maeneo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Rasilimali hizo kupitia utekelezaji wa mipango ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii "*Corporate Social Responsibility*" (CSR).

Mwenyekiti wa Kamati ya TEITAC Mhe. Balozi Wilson M. K. Masilingi alipata fursa ya kushiriki kama mjumbe wa jopo la majadiliano (*panellists*), ambapo alitumia fursa hiyo kuwaeleza washiriki hatua zilizofikiwa na Tanzania katika utekelezaji wa Sera na Sheria zinazosimamia masuala ya Uziduaji na Usimamizi wa Sekta za Madini na Gesi Asilia na kuhusu namna bora ya kuimarisha utekelezaji wa sera na kusisitiza ushirikiano wa Kimataifa na usimamizi wa utekelezaji wa Sera na Sheria kati ya nchi Wanachama wa EITI. Aidha, ilipendekezwa kuwa ni muhimu Serikali katika nchi zenye utajiri wa rasilimali kuweka mazingira wezeshi yatakayowezesha wazawa kunufaika zaidi na shughuli za uziduaji. Ili kufanikisha azma hiyo, ushauri ulitolewa kwa Serikali kuzingatia kuwajengea uwezo Wazawa Kiufundi, Kitaaluma na Kiuchumi ili waweze kutoa huduma na bidhaa zinazokidhi viwango na mahitaji ya Kampuni za Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

Vilevile, wawakilishi kutoka nchi za Zambia na Ghana waliwasilisha uzoefu wa nchi zao katika usimamizi na utekelezaji wa Matakwa husika. Uzoefu huo ulitoa fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali zinazoweza kutumiwa na nchi wanachama wa EITI kuimarisha ushiriki wa Wazawa na kuongeza mchango wa Sekta ya Uziduaji katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

3.2 Uwazi na Uwajibikaji katika Madini Muhimu na Madini ya Kimkakati- Uzoefu kutoka kwa Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa (*UN Task force on Critical Energy Transition Minerals*)

Pembezoni mwa Mkutano huo, iliandaliwa Mkutano (*VIP Round Table*) na Mwenyekiti Mhe. Balozi Wilson M.K. Masilingi alialikwa kushiriki. Mkutano huo ulilenga *UN Task Force* kutoa taarifa juu ya hatua waliyofikia juu ya namna bora ya kusimamia Madini ya Kimkakati (*Critical Energy Transition Minerals*) ambapo Duniani kwa sasa Madini hayo yana umuhimu mkubwa sana na yanagombaniwa sana kwa ajili ya kulisha Viwanda mbalimbali katika uzalishaji na uendelezaji wa Teknolojia wa Kisasa na rafiki kwa mazingira (*New Technology on Renewable*

Energy). Tanzania tunayo fursa zinazohusiana na Madini ya Kimkakati yanayohitajika katika Teknolojia za Nishati safi, kwa sababu Nchi yetu imejaaliwa madini hayo kwa wingi. Katika Mkutano huo, Mwenyekiti wa Kamati ya TEITAC-Mhe. Balozi Wilson Masilingi alimpongeza Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa hatua hiyo ya kuunda Kikosi Kazi cha Umoja wa Mataifa kuhusu "*Critical Energy Transition Minerals"* ambacho kimetoa mapendekezo mazuri. Aidha, alishauri mapendekezo hayo yaboreshwe na kuwekwa katika mfumo wa Kisheria, ili misingi hiyo (*principles*) ziwe na nguvu ya Kisheria Kimataifa (*Global Legal Framework*) badala ya utekelezaji wake kutegemea utashi wa wahusika. Kwa mfano, Haki za binadamu kama vile kuhifadhi mazingira haiwezi kutekelezwa kwa utashi.

3.3 Usalama wa Nishati Kusini-Mashariki mwa Asia: Kuimarisha Ustahimilivu katika Kipindi cha Kutokuwa na Uhakika wa Siasa za Kidunia (*Energy security in Southeast Asia: Powering Resilience in an era of geopolitical uncertainty*)

Mjadala Kuhusu usalama wa Nishati Kusini-Mashariki mwa Asia ulilenga kupata uzoefu katika nchi hizo kuhusu Usalama wa Nishati na ustahimilivu wao kwa kuzingatia mazingira ya Nchi hizo kuwa na changamoto ya Nishati na mabadiliko ya Tabia Nchi hasa wakati huu ambapo migogoro ya Kimatifa inaendelea, mabadiliko ya bei za mafuta na gesi asilia na changamoto mbalimbali zinazohusu usalama wa Nishati Duniani.

Washiriki Wakuu katika mjadala huo walikuwa kutoka nchi za Philippines, Indonesia, Timo-Leste na Papua New Guinea. Tulipata fursa ya kusikia uzoefu kutoka katika Nchi hizo juu ya Ustahimilivu wao katika kujenga uwezo wa kutoa Nishati Safi kwa wananchi wao na ya bei nafuu. Aidha, tulisikia changamoto za Utawala Bora, mapungufu katika Miundombinu, mapungufu katika Taasisi, mapungufu katika Usimamizi na Ushirikishwaji wa wadau.

Baada ya kuwasikiliza washiriki wakuu kutoka Nchi hizo, Mwenyekiti Mhe. Balozi Wilson M. K Masilingi aliombwa kutoa uchambuzi juu ya Changamoto za Utawala bora zinazoshabihiana kati ya nchi husika; wapi wanatofautiana na yapi ya kujifunza katika tofauti hizo; yapi yanaweza kuigwa na nchi ambazo mazingira yake yanaruhusu na zinakabiliwa na Changamoto zinazofanana; na je, zipo fursa za kujifunza na kushirikiana?

Mwenyekiti Mhe. Balozi Wilson M. K Masilingi katika kuchangia kama mchangiaji mkuu, aliwapongeza wote na nchi zao kwa ustahimilivu wao katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa Nishati Salama na ya bei nafuu kwa Wananchi wao. Mwenyekiti alibainisha zaidi kuwa nchi zote za Kusini Mashariki mwa Asia, kama ilivyo kwa Nchi za Afrika, zinakabiliana na Changamoto ya Miundombinu isiyotosheleza (*inadequate infrastructre*); uwezo mdogo wa Taasisi (*Limitation in Institutuion Capacity*); Changamoto ya upatikanaji wa Fedha (*Limited access to Finance*); kuyumba kisera (*Policy Instability*); na udhaifu katika Mifumo ya Utawala Bora.

Mwenyekiti wa TEITAC aliongeza kuwa jambo la kujifunza katika mjadala huo, ni kwamba ni muhimu kuhuisha malengo ya Utawala Bora na Usalama wa Nishati, ili kufikia malengo ya Usalama na Nishati (*Energy Security Objectives*), Ustahimilivu wa Nishati, mageuzi ya Kiuchumi na Kijamii katika kipindi hiki cha Siasa za Kidunia zisizotabirika. Hii itaondoa hatari ya Utawala mbaya. Badala yake Utawala Bora utavutia mitaji ya Wawekezaji ili kuongeza Ajira, Kuondoa Rushwa na Kuondoa Umaskini.

3.4 Mabadiliko mbalimbali katika Uandaaji wa Ripoti za EITI za kila Mwaka kupitia Mtaalam Elekezi (*EITI Reporting in transition:The evolving role of Independent Administrators*)

Mjadala kuhusu Uandaaji wa Ripoti za EITI za kila Mwaka kulingana na Viwango vya Kimataifa vya EITI ulifanyika. Kila nchi Mwanachama huwajibika kuandaa Ripoti hiyo. Tanzania ikiwa ni mojawapo wa Mwanachama wa EITI, ilitoa uzoefu wa hatua mbalimbali katika uandaaji wa Ripoti za EITI za kila Mwaka, kulingana na maboresho yaliyotolewa kupitia Viwango vya Kimataifa vya EITI, kama viliyopitishwa na Bodi ya EITI. Viwango hivyo vimesisitiza katika uwekaji wazi wa Mapato na Malipo yaliyolinganishwa katika Sekta ya Uziduaji na Taarifa mbalimbali kulingana na vigezo husika. Nchi Wanachama kuhakikisha wanaweka wazi taarifa zao kupitia majukwaa, tovuti zao na mitandao ya kijamii ili kuhamasisha Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali zao.

Katika majadiliano hayo, pia ilipendekezwa kuwa Nchi Wanachama wa EITI zinapaswa kuwa na Kamati imara zinazosimamia masuala ya Uwazi na Uwajibikaji (*Strong Multi Stakeholder Group - MSG*) kama TEITAC ya Tanzania. Kamati hizo zitaimarisha Mifumo ya Uwazi ya Serikali katika usimamizi wa Sekta ya Uziduaji.

Aidha, itawezesha kuwekeza katika mifumo ya Kidigitali *(digital system)* kurahisisha Wananchi wengi zaidi. Utekelezaji wa Uwazi na Uwajibikaji utawezesha uandaaji wa Ripoti za EITI ambazo zitaibua mijadala kuhusu Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika nchi husika. Aidha, itasaidia katika utungaji wa Sera zinazolinda na kuhakikisha matumizi endelevu ya Maliasili za Nchi kwa manufaa ya Wananchi.

Katika mjadala huo, Tanzania, ilitajwa kuwa mfano bora kwa Nchi zinazotekeleza muongozo wa EITI katika kuandaa Ripoti zake za EITI za kila mwaka kwa kutumia Wataalam wa ndani. Utaratibu huu unapunguza gharama za uandaaji wa Ripoti na kuimarisha umiliki wa ndani (*national ownership*) wa mchakato na matokeo ya Ripoti hizo. TEITI Sekretariati iliwasilisha Mada iliyoelezea uzoefu wa nchi ya Tanzania katika kuandaa Ripoti ya Mwaka.

3.5 Uwazi, Uongezaji Thamani na Uwekezaji Wenye Uwajibikaji

Uzoefu wa nchi ya Indonesia uliwasilishwa kuhusu umuhimu wa kuimarisha Uwazi na Uwajibikjai katika mnyororo wa thamani wa sekta ya Uziduaji, hususan katika masuala ya uongezaji thamani (*beneficiation*), Uhamishaji wa Faida kupitia Miamala baina ya Kampuni zinazohusiana (transfer pricing) na Mifumo ya Ufuatiliaji wa bidhaa na Miamala (tracing mechanisms).

Ilielezwa kuwa shughuli za uongezaji thamani zinapaswa kuzingatiwa katika utekelezaji wa Viwango vya EITI, ili kuwezesha upatikanaji wa taarifa zinazosaidia kufuatilia manufaa ya kiuchumi yanayotokana na rasilimali za nchi. Aidha, ilisisitizwa kuwa udhibiti wa *transfer pricing* unahitaji upatikanaji wa taarifa sahihi za soko, ili kuwezesha tathmini ya miamala inayofanyika kati ya kampuni zinazohusiana na kubaini uwezekano wa upotevu wa mapato ya Serikali. Kwa msingi huo, nchi wanachama wa EITI zilihimizwa kuandaa mifumo na taratibu za kuwezesha upatikanaji na matumizi ya taarifa hizo.

Kwa upande wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, majadiliano yalihusu umuhimu wa kuimarisha uwazi katika mnyororo mzima wa thamani, kuanzia shughuli za awali (upstream), shughuli za kati (midstream) hadi shughuli za mwisho (downstream). Masuala yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na uwazi kuhusu umiliki manufaa (*beneficial ownership*) na ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa wazawa (*local*

procurement), kwa lengo la kuimarisha uwajibikaji na kuhakikisha kuwa manufaa yatokanayo na Rasilimali za Uziduaji yanachangia maendeleo ya Uchumi wa Nchi.

3.6 Mipaka na Changamoto Mpya katika Utekelezaji wa EITI: Viwango cha EITI cha 2023

Majadiliano yalijikita katika masuala ya umiliki manufaa (beneficial ownership), hususan umuhimu wa kuanzisha na kuimarisha Rejista za Wamiliki manufaa katika Nchi Wanachama. Muafaka ulifikiwa kuwa kila nchi inapaswa kuwa na Rejista ya Wamiliki manufaa inayohifadhi taarifa sahihi na kuhakikiwa mara kwa mara. Aidha, changamoto kubwa iliyobainishwa ni mgongano unaoweza kujitokeza kati ya masharti ya Kisheria yanayolinda usiri wa Taarifa na yale yanayohitaji taarifa hizo kuwekwa wazi kwa madhumuni ya Uwazi na Uwajibikaji, ili kupambana na Rushwa na utakatishaji pesa. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, ilisisitizwa kuwa Nchi Wanachama zinapaswa kupitia na kuoanisha mifumo yao ya Kisheria na Kiutawala, ili kupata mizania sahihi kati ya wajibu wa kulinda usiri wa Taarifa na mahitaji ya kuzitoa kwa maslahi ya umma, kwa kuongozwa na Kiwango cha EITI cha mwaka 2023.

3.7 Umuhimu wa Takwimu kwa Ajili ya Utungaji wa Sera na Kufanya Maamuzi

Mkutano ulijadili umuhimu wa takwimu katika utungaji wa sera, kufanya maamuzi na matumizi yake kwa ujumla. Ilielezwa kuwa, licha ya takwimu kuwa nyenzo muhimu katika kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Sekta ya Uziduaji, Nchi nyingi Wanachama zinakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazokwamisha matumizi yake. Aidha, ilisisitizwa kuwa takwimu ni nyenzo muhimu katika kuanzisha mijadala yenye ushahidi, kuimarisha ushiriki wa wadau na kuwezesha maamuzi yanayotegemea taarifa sahihi. Katika hilo, nchi ya Ufilipino ilitolewa kama mfano wa nchi yenye mfumo maalumu ya takwimu unaojulikana kama EIDAn, unaolenga kurahisisha upatikanaji wa taarifa na kuimarisha matumizi ya takwimu katika sekta ya uziduaji.

3.8 Mambo ya Kujifunza Kutokana na Uzoefu wa Nchi Mbalimbali

Katika mjadala huu, ilisisitizwa kuwa uwekezaji katika mpito wa nishati (energy transition) ni muhimu. Aidha, washiriki walibadilishana uzoefu kuhusu usimamizi wa

rasilimali, uwazi wa taarifa, ubora wa takwimu na changamoto za utekelezaji wa viwango vya EITI katika nchi mbalimbali, kama ifuatavyo:

Nchi ya Mongolia: walitoa taarifa kuwa Bunge la Mongolia limeidhinisha sera mpya zinazohusu misitu, maji na wanyamapori, ikiwemo uwindaji, ili masuala hayo yajumuishwe katika wigo wa utekelezaji wa viwango vya EITI. Aidha, tangu mwaka 2017, zoezi la ulinganishi wa taarifa za malipo na mapato (reconciliation) limekuwa likitekelezwa na Sekretarieti ya Kitaifa baada ya kuondolewa kwa Mshauri Huru. Vilevile, mwaka 2019, Katiba ya nchi hiyo ilifanyiwa marekebisho ili kutambua haki ya wananchi kupata taarifa kuhusu rasilimali zao.

Nchi ya Mali: Walishauri kuwa kutokana na uzoefu wa Nchi hiyo, usimamizi bora wa rasilimali za nchi unahitaji kuwepo kwa kanuni za maadili (Code of Conduct) au utaratibu mwingine unaofanana na huo, utakaosaidia kuimarisha Uadilifu na Uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali hizo.

Nchi ya Jamhuri ya Kongo: Waliwasilisha taarifa kuhusu masuala ya umeme na mazingira, pamoja na changamoto za uwekaji wazi wa mikataba inayofungwa kati ya Serikali na Kampuni. Walieleza kuwa bado wanakabiliana na changamoto ya kubainisha wajibu wa kuweka Mikataba hiyo wazi, hususan iwapo jukumu hilo linapaswa kutekelezwa na kampuni husika au Serikali. Aidha, walieleza kuwa kuna makundi yanayopinga au kuzuia juhudi za kuweka mikataba hiyo wazi.

Nchi ya Gabon: Taarifa ya Nchi ya Gabon ilijikita katika umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji na utoaji wa taarifa kuhusu masuala la ushiriki wa wazawa (local content), uzalishaji wa Hewa Ukaa (carbon emmission) na masuala mengine yanayohusiana na sekta ya uziduaji, ili kuhakikisha masuala hayo yanazingatiwa katika mifumo ya uwazi na uwajibikaji wa sekta hiyo. Kuhusu ubora na uaminifu wa takwimu, ilipendekezwa kuwa wajumbe wa Multi-Stakeholder Group – MSG wapewe mafunzo ya kutosha, ili kuimarisha uwezo wao wa kutathmini taarifa zinazowasilishwa. Aidha, ilisisitizwa umuhimu wa kuwateua wawakilishi wenye uelewa wa kutosha kuhusu hali halisi ya sekta na masuala yanayojadiliwa. Ilibainishwa pia kuwa kufikia maridhiano ndani ya MSG kumekuwa changamoto kutokana na tofauti za uwezo wa kitaalamu na uwakilishi kati ya Serikali, kampuni na asasi za kiraia.

3.9 Uwazi kwa Ustawi wa Pamoja (Transparency for Shared Prosperity)

Nchi ya Uganda: Waziri wa Nchi (Mipango) na Mwenyekiti wa EITI Uganda alieleza kuwa Nchi hiyo inatambua mchango wa rasilimali za Mafuta na Gesi katika kuongeza mapato ya Serikali na kugharamia utekelezaji wa bajeti ya Taifa. Alibainisha kuwa Uganda inafuatilia mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya Mafuta na Gesi, kuanzia shughuli za utafutaji na uzalishaji (upstream) hadi usafirishaji, uchakataji na usambazaji wa bidhaa za mafuta na gesi (downstream). Aidha, alieleza kuwa kwa mujibu wa sheria za nchi hiyo, asilimia 0.8 ya mapato husika hutengwa kwa ajili ya maendeleo ya miundombinu.

Nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC): Bi. Marie-Chantal Kaninda – Rais wa Glencore DRC na Mwenyekiti wa Bodi ya Kamoto Copper Company alisisitiza kuwa uwazi na kuaminiana kati ya Serikali, Kampuni na Wadau wengine ni msingi wa uwajibikaji na upatikanaji wa manufaa ya pamoja katika Sekta ya Uziduaji. Alieleza kuwa kampuni inaweza kuchangia ustawi wa jamii kupitia utoaji wa ajira na kufuata matakwa ya kisheria katika shughuli zake. Kwa mfano, alibainisha kuwa Kampuni husika ina wafanyakazi 18,000, ambapo asilimia 90 ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Aidha, alisisitiza umuhimu wa kampuni kutimiza wajibu wake wa kulipa Kodi na tozo zinazostahili kwa Serikali, kwa kuzingatia Sheria na masharti yanayoongoza shughuli zake.

4.0 MKUTANO WA UJUMBE WA TANZANIA NA BALOZI WA TANZANIA NCHINI UBELIGIJI

Ujumbe wa Tanzania ulifanya Kikao na Balozi wa Tanzania nchini Ubeligiji- Mhe. Balozi Jestas Nyamanga. Kikao hicho kilishirikisha Watumishi wa Ubalozi. Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Kamati ya TEITAC alimshukuru Mheshimiwa Balozi kwa mapokezi mazuri na ukarimu wa hali ya juu kuanzia ujumbe wetu ulipowasili uwanja wa ndege Brussels na Ubalozini. Mwenyekiti alieleza lengo la Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Kumi wa Kimataifa wa EITI, nchi yetu ikiwa ni Mwanachama wa Asasi ya Kimataifa ya EITI. Aidha, tuliweza kuwafahamisha kwa ufupi majukumu ya Taasisi ya TEITI na kueleza hatua iliyofikiwa na Nchi yetu katika kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia.

Kwa upande wake, Mhe Balozi wa Tanzania nchini Ubeligiji, alipongeza juhudi zinazofanywa katika kuhakikisha kuwa Rasilimali za Nchi yetu zinasimamiwa kwa

Uwazi na Uwajibikaji, ili zinufaishe Watanzania wote. Aidha, Mhe. Balozi alisisitiza umuhimu wa TEITAI kujikita zaidi katika masuala ya usimamizi wa Madini Muhimu na ya Kimkakati kwa sabau nchi yetu imebarikiwa kuwa na Madini hayo na kuna ongezeko la mahitaji ya madini hayo Duniani kwa sasa. Alieleza kwamba Madini hayo yana nafasi muhimu katika maendeleo ya Teknolojia za nishati safi na katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi kupitia matumizi ya nishati Rafiki kwa Mazingira. Aidha, Mheshimiwa balozi alituahidi kushirikiana na TEITAI katika kuhakikisha majukumu ya Taasisi yanatekelezeka kwa ufanisi. Mheshimiwa Balozi alisisitiza umuhimu wa ushirikishwaji Wazawa katika Sekta ya Uziduaji (Local Content), ili Wazawa wanufaike zaidi kupitia rasilimali zao.

5.0 MKUTANO WA UJUMBE WA TANZANIA NA MTENDAJI MKUU WA SEKRETARIAT YA EITI BW. MARK ROBINSON

Ujumbe wetu pia ulikutana na Mtendaji Mkuu wa EITI- Bw. Mark Robinson na Watendaji wengine wa Sekretariat ya EITI. Mwenyekiti wa TEITAC alimshukuru Mtendaji Mkuu wa EITI kwa kutenga muda wake kukutana na ujumbe wetu. Aidha, aliishukuru Sekretariet nzima ya EITI kwa ushirikiano wanaotoa kwa nchi yetu katika utekelezaji wa shughuli za kusimamia Uwazi na Uwajibikaji katika Uzinduaji wa rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania.

Mtendaji Mkuu wa Sekretariat ya EITI alipongeza juhudi za Tanzania katika utekelezaji wa vigezo vya kimataifa vya EITI ambapo ilielezwa kuwa tangu Tanzania ijiunge na Asasi hiyo ya EITI utekelezaji wa vigezo hivyo unaridhisha na unaendelea kuimarika mwaka hadi mwaka. Aidha, aliipongeza Tanzania kwa kuchukua juhudi za kuhakikisha Ripoti za TEITI za kila Mwaka zinaandaliwa na Wataalam wa ndani.

Aidha, Mtendaji Mkuu wa EITI alieleza kuwepo kwa mradi mpya unaohusu usimamizi wa Madini muhimu na ya Kimkakati (*Critical Energy Transition Minerals*), ambao utasimamiwa/kufadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU). Aliongeza kwamba makubaliano yatasainiwa hivi karibuni, ambapo inategemea Tanzania itakuwa miongoni mwa wanufaika wa mradi huo. Mtendaji Mkuu wa Sekretariat ya EITI alisema EITI ipo tayari kushirikiana na Tanzania katika zoezi la tathmini ya utekelezaji wa shughuli za EITI litakaofanyika Julai, 2027. Alitufahamisha kuwa Sekretareti ya EITI wanatarajia kutembelea Tanzania mwishoni mwa mwezi Novemba, 2026 kwa ajili ya maandalizi ya zoezi hilo.

Mwenyekiti wa Kamati ya TEITAC aliishukuru EITI kwa kuendelea kuipa Tanzania ushirikiano wa kutosha katika kutekeleza majukumu yake. Alimhakikishia kwamba TEITAI ipo tayari kushirikiana na EITI, ili kukidhi utekelezaji wa Vigezo vya Kimataifa vya EITI kikamilifu.

6.0 USHIRIKI WA TANZANIA KATIKA MAONESHO

Sambamba na Mkutano wa Kimataifa wa EITI, Ujumbe wa Tanzania ulishiriki katika maonesho ambapo Nchi Wanachama wa EITI walipata fursa ya kuonesha bidhaa na huduma wanazozitoa katika kuelimisha na kuhamasisha Uwazi na Uwajibikaji katika Uziduaji wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia. Nchi zaidi ya 30 zilishiriki katika maonesho hayo. Washiriki wengi walivutiwa na huduma na bidhaa zinazotolewa na Tanzania ikiwemo uandaaji wa ripoti za TEITAI kwa lugha za alama kwa wanachi wetu wenye changamoto za uoni hafifu. Aidha, washiriki walivutiwa na juhudi za Tanzania katika kuandaa ripoti za EITI za kila Mwaka kupitia Wataalam wa ndani. Aidha, utekelezaji wa takwa la uwekaji wazi wa Mikataba na Majina ya Wamiliki wa Hisa katika Kampuni zinazojihusisha na Sekta ya Uziduaji ulipongezwa na kuelezwa kuwa mfano wa kuigwa.

7.0 USHAURI

7.1 Tunashauri Taasisi huru ya Serikali TEITAI itengewe Bajeti ya kutosha na kupewa Ofisi zinazotosheleza kuweza utekelezaji wa Majukumu yake Kitaifa na Kimataifa.

7.2 Tunashauri wigo wa usimamizi wa Uwazi na Uwajibikaji upanuliwe, ili kujumuisha Rasilimali za Bahari (Uvuvi); Misitu na Wanyapori. Mikakati mizuri inayotekelezwa sasa na Serikali yetu, ni vema ikasimamiwa kwa Uwazi na Uwajibikaji zaidi, ili wananchi wajue mafanikio makubwa yaliyopatikana.

7.3 Tunashauri hatua madhubuti na Shirikishi zichukuliwe kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Madini Muhimu na ya Kimkakati (*Critical Energy Transition Minerals*) yafuatayo:Lithiamu ambayo ni muhimu katika utengenezaji wa Betri za Magari ya Umeme na Madini mengine kama vile Cobalt, Graphite, Manganese, Copper na Nickel ambayo ni muhimu sana katika matumizi mbalimbali kama vile kutengeneza teknolojia ya Nishati safi na salama kwa mazingira na masuala ya Ulinzi wa Nchi.

7.4 Tunashauri nchi yetu itekeleze kwa haraka Mkakati wa kujenga Viwanda vya kuongeza thamani katika Madini muhimu ya kimkakati Duniani kwa kuzingatia Dira ya 2050 ili Madini ya Kimkakati yatumike kuongeza ajira, ukuaji wa uchumi imara, kuondoa Umaskini, Rushwa na Maendeleo endelevu.

7.5 Tunashauri Viongozi, Wataalam wa Serikali Waandamizi na Wabunge wawezeshwe ili waweze kushiriki Mikutano ya Kimataifa, ikiwemo ya EITI kubadilishana uzoefu wa nchi zingine juu ya namna ya kulinda maslahi ya nchi zilizobarikiwa kuwa na Madini ya Kimkakati ambayo Mataifa makubwa yanashindania wakati mwingine kwa kutumia mbinu chafu zinazohatarisha usalama wa nchi zenye rasilimali hizo.

8.0 HITIMISHO

Ushiriki wetu katika mkutano wa kumi (10) wa EITI imekuwa fursa nzuri ya kueleza hatua zinazo chukuliwa na Nchi yetu kuimarisha Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia katika nchi yetu. Aidha, imekuwa ni fursa ya kujifunza kutoka katika uzoefu wa nchi nyingine na wadau wa Sekta ya Uziduaji, yakiwemo Mashirika yasiyo ya Serikali.

Ni muhimu kuendelea Kuimarisha mfumo na taratibu za Uwazi na Uwajibikaji katika Usimamizi wa Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia, ili kuhakikisha kuwa utajiri wa rasilimali hizo unaleta manufaa halisi kwa wananchi. Lazima tuendelee kuhamasisha Uwazi katika mnyororo mzima wa kuongeza thamani katika Sekta ya Uziduaji, kuanzia hatua ya Utafutaji, Uchimbaji, Uchakataji hadi Sokoni. Tuendeleze ushirikiano na Jumuiya ya Kimataifa katika kubadilishana uzoefu baina ya Nchi Wanachama wa EITI, kuhusu mbinu bora za kusimamia Rasilimali Madini, Mafuta na Gesi Asilia kwa manufaa ya Wananchi wote. Tuweke mkazo katika kuhamasisha matumizi ya Akili unde na kuimarisha mifumo yetu ya kidigitali (*Digital Transformation*) katika usimamizi wa shughuli za Uwazi na Uwajibikaji, hususan katika uchambuzi wa taarifa na takwimu, ufuatiliaji wa mwenendo wa Mapato na kubaini maeneo yanayohitaji kuimarishwa katika usimamizi wa rasilimali za Nchi yetu.

Tunaomba Kuwasilisha.

Kiambatisho 1: BARUA YA KATIBU MTENDAJI WA EITI KUSHUKURU USHIRIKI WA TANZANIA

Extractive Industries Transparency Initiative

20 October 2026

Ambassador Wilson Mutagaywa Kajumula Masilingi
Chair, TEITI Multi-Stakeholder Group
United Republic of Tanzania

2026 EITI Global Conference

Dear Ambassador Masilingi,

The EITI International Secretariat wishes to express its sincere appreciation for your participation to the 2026 EITI Global Conference in Brussels, Belgium, as well as the insightful remarks you shared during our bilateral meeting. The conference brought together over 1000 delegates from governments, companies, civil society and partner organisations around the theme "Transparency for shared prosperity". Your leadership helped reinforce the EITI community's commitment to strengthening transparency, accountability and responsible resource governance.

We particularly welcomed TEITI initiative to produce EITI Reporting and develop an in-house Digital Reporting System, as showcased in the Peer Learning Day, and for the commitment demonstrated by your leadership at the MSG to advance on the corrective actions from the previous Validation.

Our Africa team remains fully committed to providing implementation support to Tanzania, as your multistakeholder group works diligently towards upcoming Validation. We look forward to our continued collaboration.

Thank you again for your support in making the 2026 EITI Global Conference a success.

Sincerely,

Mark Robinson
Executive Director
Extractive Industries Transparency Initiative

cc: Ms. Mariam Mgaya, National Coordinator, TEITI
Mr Erick Ketagory, Accountability and Transparency Manager, TEITI

EITI International Secretariat
Phone: +47 222 00 800 • E-mail: secretariat@eiti.org • Twitter: @EITIorg
Address: Rådhusgata 26, 0151 Oslo, Norway • www.eiti.org

Kiambatisho Na 2: *WAJUMBE WA TEITAC WALIOSHIRIKI*



Picha Na. 1: *Ujumbe wa Tanzania Ulioshiriki Mkutano wa Kumi wa Kimataifa wa EITI, Kutoka Kulia, Bi. Julieth N. Moshi, Bw. Bakari I. Birika, Bi. Mariam S. Mgaya Mtendaji Mkuu wa TEITAI, Mhe. Balozi Wilson M. K. Masilingi Mwenyekiti wa TEITAC, Bw. Adam A. Anthony Mjumbe wa TEITAC na Bw. Erick P. Ketagory.*



Picha Na. 2: *Mwenyekiti wa TEITAC Mhe. Balozi Wilson M.K. Masilingi akieleza hatua zilizochukuliwa na nchi yetu*



Picha Na. 3: *Mwenyekiti wa TEITAC Mhe. Balozi Wilson M.K. Masilingi akichangia katika mjadala kuhusu Ustahimilivu katika Usalama wa Nishati katika Nchi za Kusini – Mashariki mwa Asia na Mambo ya Kujifunza katika Ushiriki wa Kimataifa*



Picha Na.3: *Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu Bw. Bakari Birika akiwasilisha Mada kuhusu uzoefu wa Tanzania katika uandaaji wa Ripoti na Ujengaji wa Mfumo wa Uandaaji wa Ripoti (EDR-MIS)*



Picha Na. 4: *Balozi wa Tanzania Nchini Ubeligiji Mhe. Balozi Jestas Nyamanga aliyesimama katikati kushoto kwa mhe. Mwenyekiti wa TEITAC katika picha ya pamoja na Ujumbe wa Tanzania*